TANGAZO LA SERIKALI NA. 680 La Tarehe 21/8/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 80 )*

SHERIA NDOGO ZA HIFADHI ZA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA ZA MWAKA, 2020

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hii itaitwa Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Manispaa za Mpanda, 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo:

"eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji unaozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"maeneo ya malisho" maana yake ni sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri au Kijiji kuwa

maeneo ya malisho ya mifugo;

Sura ya 191

"mazingira" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mifugo" maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

Sura 323

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia kumi na miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia hamsini au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo imetangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

Masharti kuhusu ufugaji

3.- (1) Mtu yeyote anayefuga katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;

(b) kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(c) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(d) kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri;

(e) kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;

(f) kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(g) kuweka alama kwenye mifugo yake na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;
(h) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
(i) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyohitajiwa na Halmashauri;
(j) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:
(a) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
(b) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;
(c) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;
(e) kufuga mifugo kwa zaidi ya idadi iliyoelekezwa na Halmashauri; au
(f) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata mifugo inayokutwa katika maeneo yasiyoruhusiwa kuchunga, kulisha au kunywesha mifugo.

(4) Endapo mmiliki wa mifugo iliyokamatwa kwa mujibu wa aya ya (c) kifungu kidogo cha (2) na

kifungu kidogo cha (3) atashindwa kulipa faini iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii, Halmashauri inaweza, baada ya kupata amri ya Mahakama, kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mifugo hiyo na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo baada ya kutoa gharama za ukamataji, utunzaji wa mifugo na Mahakama.

Masharti kuhusu kilimo

4.- (1) Mtu yeyote anayelima katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) taratibu za kilimo kwa kuzingatia kalenda ya kilimo ya Halmashauri na kwa kuzingatia Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi na mazingira;

(b) kutolima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa au maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira;

(c) kutotumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri; na

(d) kutosafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto, isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(2) Kibali cha kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaoruhusiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia kumi na mbili asubuhi hadi saa nne kamili asubuhi na saa kumi na mbili jioni hadi saa moja kamili usiku.

(4) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya

yafuatayo:

(a) kutozingatia kalenda ya kilimo ya Halmashauri;

(b) kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, milima, mabwana au maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira;

(c) Kutumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri; au

(d) kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto bila ya kuwa na kibali au nje ya muda ulioruhusiwa chini ya Sheria Ndogo hii.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

5.- (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchimba mchanga, kokoto, mawe, udongo au madini yoyote ya ujenzi kwa madhumuni ya kibiashara karibu na makazi ya watu, maeneo ya hifadhi, kandokando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa vyanzo vya maji

6.- (1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa:

(a) kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Halmashauri;

(b) kutoishi katika eneo la hifadhi au chanzo cha maji;

(c) kutolima, kutokata miti, kutochunga mifugo au kutofanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote eneo lililotangazwa kuwa eneo la hifadhi au

chanzo cha maji; au

(d) kutoelekeza mabomba ya maji machafu au kujisaidia kwenye mito, mabwawa, maziwa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji;

(e) kujimilikisha eneo ambalo ni chanzo cha maji cha umma.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa misitu

7.- (1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa:

(a) kutokata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri;

(b) kutochoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika eneo la Halmashauri;

(c) kutovuna miti isipokuwa kwa kibali maalum cha Halmashauri; au

(d) kutovuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe malum.

(2) Uchomaji wa mkaa utafanyika kwa kibali maalum cha Halmashauri katika maeneo yaliyotengwa mahsusi kwa ajili hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Utupaji wa taka

8.- (1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakiwa kufanya yafuatayo:

(a) kuwa na shimo au chombo maalum cha kuhifadhi taka ngumu na laini; na

(b) kuwa na choo safi na salama.

(2) Halmashauri itatakiwa kutenga eneo maalum

kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo hilo.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa jumla

9.- (1) Wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira yameharibiwa watakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida eneo hilo kwa kupanda miti na kuendelea kutoharibu mazingira ili kuwezesha uoto au mazingira yarudi katika hali yake ya kawaida kwa kadri watakavyoelekezwa na Halmashauri.

(2) Wakazi wa eneo ambalo moto umetokea unaotishia maisha ya watu, mali au mazingira watakuwa na wajibu wa kushiriki kuzima moto huo kwa kadri watakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Kila Halmashauri ya Serikali ya Kijiji itatakiwa kutenga eneo la hifadhi ya misitu, kusimamia kila mwanakijiji anapanda miti isiyopungua kumi katika eneo la makazi na miti hamsini katika eneo la shamba, kila shule au taasisi ya umma inapanda miti ya kukinga upepo kuzunga majengo.

(4) Mtu yeyote atakayeshindwa, bila sababu za msingi, kutekeleza maelekezo ya Halmashauri chini ya kifungu kidogo cha (1), (2) na cha (3) atakuwa ametenda kosa.

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atahukumiwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha Kosa

11. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo mtu atakiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa kumtoza kiasi cha shilingi elfu thelathini baada ya kujaza fomu maalum iliyoambatishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

*Tangazo La Serikali Na. 680 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 3(4))*

SEHEMU YA KWANZA

VIWANGO VYA FAINI KWA MFUGO AU MIFUGO INAYOZURURA NDANI YA ENEO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA

| Na | AINA YA MFUGO | KIWANGO CHA FAINI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | NG'OMBE | 5000/= kwa kila n'gombe |
| 2 | MBUZI | 3000/= kwa kila mbuzi |
| 3 | KONDOO | 3000/= kwa kila kondoo |

SEHEMU YA PILI

VIWANGO VYA FAINI KWA MFUGO AU MIFUGO INAYOLISHWA AU KUNYWESHWA KATIKA SEHEMU ZISIZORUHUSIWA

| Na | AINA YA MFUGO | KIWANGO CHA FAINI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | NG'OMBE | 5000/= kwa kila n'gombe |
| 2 | MBUZI | 3000/= kwa kila mbuzi |
| 3 | KONDOO | 3000/= kwa kila kondoo |

SEHEMU YA TATU

VIWANGO VYA FAINI KWA MFUGO AU MIFUGO KUINGIA KATIKA ENEO LA HALMASHAURI BILA KIBALI

| Na | AINA YA MFUGO | KIWANGO CHA FAINI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | NG'OMBE | 5000/= kwa kila n'gombe |
| 2 | MBUZI | 3000/= kwa kila mbuzi |
| 3 | KONDOO | 3000/= kwa kila kondoo |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ....................................................................... nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya.......................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kwamba tarehe ..........ya Mwezi ................... Mwaka................. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ya Mwaka 2020.
Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: ....................................................
Saini: ...................................................

Mbele ya:
Jina……...............................................
Cheo: .................................................
Saini: .................................................
Tarehe: .............................................

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa Mpanda imegongwa katika sheria Ndogo hizi kufuatia azimio Na: MUHT/MMC/BARAZA/02/2018/2019/AGD:13 la kikao cha Halmashauri ya Manispaa Mpanda kilichofanyika tarehe 25 Mwezi Januari, 2019, na imebandikwa na kushuhudiwa na;

MICHAEL F. NZYUNGU
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Manispaa Mpanda*

WILLIAM P. MBOGO
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa Mpanda.*

S.L

NAKUBALI

Dodoma,
Tarehe 5 Agusti,2020

Mhe.SELEMANI S. JAFO (MB.)
*Waziri Ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.*